

»Usimamizi wa Nguruwe«

Kwa kuwa ni biashara yenye faida kubwa, ubora na wingi wa bidhaa zinazopatikana kwa ufugaji wa nguruwe hubainishwa na mbinu ya uzalishaji inayotumika.

Kuna hatua 4 za utunzaji wa nguruwe waliozaliwa; hatua ya kwanza ni kukata kitovu na kukiweka kwenye myeyusho wa iodini, pili ni kupunguza meno, tatu ni kumdunga mwana-nguruwe 1 ml ya dawa ya ayon dextran ndani ya misuli, na hatua ya mwisho ni kumpa nguruwe vichochezi vyta ukuaji.

Utunzaji wa nguruwe

Kwa hatua ya kwanza, kata kitovu cha nguruwe na uache inchi 2 na upake mmumunyo wa iodini ili kuzuia bakteria kuingia na hivyo kudhibiti ugonjwa unaosababisha mkusanyiko wa damu kwenye viungo, na hivyo kusababisha uvimbe wa viungo vyta nguruwe.

Zaidi ya hayo, punguza meno kwa kutumia mkasi maalum ili kuzuia majeraha. kwa sababu wana- nguruwe huzaliwa na upungufu wa madini ya chuma, dunga 1 ml ya dextran kwenye misuli ya nguruwe ili kuongeza chuma.

Hatimaye, mpe mnyama 2ml ya kichochezi cha ukuaji ili kumtolea vitamini na madini.